

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA NISHATI

SHIRIKA LA MAENDELEO YA PETROLI
TANZANIA



TAARIFA KWA UMMA

08/07/2021

Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC), linakanusha taarifa iliyotoka katika vyombo vya habari vya ITV na Radio One, kwamba mnamo tarehe 7 Julai 2021 kulitokea mlipuko wa gesi katika kiwanda cha Dangote Mkoani Mtwara na kusababisha kifo cha mtu mmoja na majeruhi kumi na mbili (12).

Shirika linataarifu umma hakuna mlipuko wowote wa gesi asilia uliotokea katika miundombinu ya gesi na kwamba miundombinu ipo salama.

Taarifa kutoka kiwanda cha Dangote zinaeleza kwamba, kulitokea ajali wakati wa kufanya matengenezo ya tanuru la Kiwanda, ambapo vumbi la moto lililokuwa kwenye tanuru liliangukia mafundi na kusababisha kifo cha mtu mmoja na majeruhi kumi na mbili (12).

Shirika linawatoa wasiwasi watumiaji wa gesi kuwa miundombinu ipo salama, na waendeleo kutumia gesi asilia bila hofu yoyote.

Imetolewa na;

Kitengo cha Uhusiano na Mawasiliano

Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC)

S.L.P 1191

DODOMA

Simu: +255262323519

Barua pepe: info@tpdc.co.tz

Tovuti: www.tpdc.co.tz

Tel: +255 22 2200103/4 2200112

Fax: +255 22 22 2200113